(vi) Kuteua wakaguzi wa mashamba ya korosho na vitalu vya miche ya mikorosho, korosho ghafi na zilizobanguliwa, viwanda vya kubangua korosho na ghala za kuhifadhia korosho.

(vii) Kuiwakilisha Serikali ndani na nje ya nchi katika masuala yanayohusu tasnia ya korosho.

(viii) Kusuluhisha migogoro kati ya wakulima, wafanyabiashara, wabanguaji, waendesha ghala wengine katika mnyororo wa biashara ya korosho nchini.

(ix) Kwa idhini ya Waziri wa Kilimo kufanya biashara ya korosho ikiwa ni kwa maslahi ya maendeleo ya tasnia ya korosho nchini.

(x) Kufanya chochote ambacho kwa maoni ya Bodi ya Wakurugenzi kimehesabiwa kuwezesha na kuongeza utekelezaji mzuri wa majukumu ya Bodi ya Korosho Tanzania.

## Shughuli za Uwezeshaji (Facilitation)


(i) Kutoa leseni au vibali vya ununuzi, ubanguaji na usafirishaji wa korosho nchini.

(ii) Kuunganisha juhudi na jitihada za wadau katika kupanua na kuboresha tasnia ya korosho nchini.

## Shughuli za Uhamasishaji (Promotion)

(i) Kuhamasisha uundwaji wa vikundi vya wadau kwa ajili ya uendelezaji wa zao la korosho nchini.

(ii) Kutoa msaada wa vifaa na/au huduma kwa ajili ya uendelezaji wa zao la korosho nchini.



## VIPAUMBELE VYA BODI YA KOROSHO

(i) Kuratibu miradi ya maendeleo ya kilimo kwa lengo la kuongeza tija katika maeneo yanayolimwa kiasili zao la korosho na kukuza uzalishaji katika maeneo mapya;

(ii) Kuratibu huduma za ugani zinazotolewa kwa wakulima kwa kushirikiana na Taasisi nyingine kama vile TARI - Naliendele, TPRI Mamlaka za serikali za mitaa, Wasambazaji wa pembejeo, Vyama vikuu vya ushirika, Washirika wa maendeleo na kadhalika;

(iii) Kuratibu mfumo wa ununuzi wa korosho na upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima na kwa bei rafiki;

(iv) Kuhamasisha usindikaji wa korosho ili kuongeza thamani na kukidhi mahitaji ya masoko ya ndani na ya kimataifa;

(v) Kutafuta masoko ya ndani na ya kimataifa ya korosho ghafi na korosho karanga ili kuongeza pato la taifa kupitia zao la korosho;

(vi) Kukusanya na kusambaza habari au takwimu zinazohusu maendeleo ya korosho ghafi /korosho karanga na tasnia kwa ujumla.

**BODI YA KOROSHO TANZANIA**



# IJUE BODI YA KOROSHO

P. O. Box 533, Mtwara, Tanzania
Tel: (023) 2333303 | Fax (023) 2333536
www.cashew.go.tz








## UTANGULIZI

Bodi ya Korosho Tanzania ni taasisi ya umma iliyoko chini ya Wizara ya Kilimo iliyoanzishwa kwa Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2010. Bodi hii imekasimiwa jukumu la kusimamia maendeleo ya zao la korosho katika ngazi zote za uzalishaji, ubanguaji/usindikaji, masoko na utafiti ili kuhakikisha kuwa zao la korosho linatoa mchango wake katika kuinua pato la mkulima wa zao hili na Taifa kwa ujumla.

***Dira (Vision)*** ya Bodi ya Korosho ni kuwa Taasisi ya ushindani kwa kutoa ushauri wa sera, usimamizi, ushauri wa kitaalam wenye tija kiuchumi na muendelevu katika tasnia ya korosho.

***Dhima (Mission)*** ya Bodi ya Korosho ni kuhamasisha, kusimamia masuala yote yenye maana na tija katika kuendeleza tasnia ya korosho Tanzania.

***Maadili (Values):*** intergrity, impartiality in Service; Pursuit of Excellence in service, diligence on duty.

## Historia ya Bodi ya Korosho Tanzania

Bodi ya Korosho Tanzania imepitia mabadiliko mbalimbali ya kisheria. Mabadiliko hayo yalienda sanjari na mabadiliko ya majina kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka 1962 'Southern Region Cashewnut Board';

(ii) Mwaka 1963 'Southern Agricultural Products Board';

(iii) Mwaka 1964 'National Agricultural Products Board';

(iiii) Mwaka 1973 'Cashewnut Authority of Tanzania' (Cashewnut Industry Act 1973);

(v) Mwaka 1984 'Tanzania Cashewnut Marketing Board' (Act No. 21 of 1984);

(vi) Mwaka 1993 Cashewnut Board of Tanzania (Ammendement to Act No. 21 of 1984). na

(vii) Mwaka 2009 Cashewnut Board of Tanzania (Cashewnut Industry Act No. 18 of 2009).

## Muundo wa Bodi ya Korosho Tanzania

Bodi ya Korosho Tanzania inaundwa na Bodi ya Wakurugenzi, Mkurugenzi Mkuu, Kitengo cha Sheria, Kitengo cha Mkaguzi wa Ndani, Kitengo cha Manunuzi na ugavi, Kurugenzi ya Fedha na Utawala, Kurugenzi ya Kilimo na Ubaguaji, Kurugenzi ya Masoko na udhibiti ubora pamoja na matawi tano (5) yaliyopo Dar es Salaam, Tanga, Tunduru, Lindi na Manyoni pamoja na kituo kimoja (1) cha Morogoro.

## Majukumu ya Bodi ya Korosho Tanzania

Majukumu ya Bodi ya Korosho yapo kwa mujibu wa sheria tajwa hapo juu. Majukumu hayo yamegawanyika katika makundi matatu kama ifuatavyo:-

## Shughuli za Usimamizi (Regulatory)

(i) Kuishauri Serikali juu ya Sera na Mikakati ya maendeleo ya tasnia ya korosho nchini ili kuhimili ushindani wa soko la ndani na la nje.

(ii) Kukusanya, kuchambua, kuhifadhi, kusambaza na kutumia takwimu zinazohusu tasnia ya korosho nchini.

(iii) Kusajili wadau mahsusi (Cashewnut dealer) ikiwa ni pamoja na wakulima wa korosho nchini.

(iiii) Kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni, miongozo na taratibu katika ulimaji, ubanguaji, usafirishaji,uhifadhi, na uuzaji wa korosho.

(v) Kudhibiti ubora wa korosho ghafi na zilizobanguliwa pamoja na bidhaa zake.